

# Waziri Ndaki awataka wauza kuku kujisajili

NA ASHURA ASSAD

**W**AZIRI wa Mifugo na Uvubi, Mashimba Ndaki, amesema sekta ya mifugo imekua kutoka asilimia tano mwaka 2018-2019 hadi asilimia 7.4, mwaka huu.

Pia, amewataka wafugaji wote wanaouza kuku wa nyama, kujisajili bodi ya nyama kwa ajili ya biashara, vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakayekaidi.

Kauli hiyo allitoa jijini Dar es Salaam, jana, wakati wa mkutano wa wizara hiyo na wafugaji wa kuku wa nyama nchini.

Ndaki, alisema sekta ya ufugaji ni muhimu kwa pato la nchi na kuwataka

wataalamu wa mifugo kufanya utafiti wa mifugo kwa kuwalenga wafugaji ili kubaini changamoto zao, badala ya kuwatumia wasomi.

"Tuache kufanya tafiti kwa kuwatumia bwana shamba na bibi shamba, ambao hawafikishi ujumbe kwa wafugaji kuhusu elimu dhidi ya tafiti zilizofanyika," alieleza.

Aliitaka wizara hiyo kutotoa vibali kiholela kwa kampuni zinazouza vifaranga vyat kuku na chakula, badala yake iwafulatille wahusika.

Ndaki, amewataka viongozi wa wizara hiyo, kuacha kukaa ofisini, watoke kusikiliza changamoto za wananchi na kuzifanyia kazi.

Amezitaka kamati za ulinzi na usalama llala na Temeke, kuwaondoa

mawakala waliopo maeneo ya Tazara, kwa kuwa eneo hilo siyo mnada wa kuuza vifaranga vyat kuku na wapo eneo hilo kinyume cha sheria.

Kaimu Msajili wa Bodii ya Nyama, Imani Sichwale, aliwataka wafugaji hao kuacha kufuga kuku kwa mazoea, badala yake wafuge kitaalamu kwa kuweka bajeti ya utugaji kwa lengo la kukuza tasnia yao.

Aliwataka wataalamu wa wizara hiyo kutoka elimu mara kwa mara kwa wafugaji wa kuku wa nyama kwa kuwa wengi hawana elimu ya ufugaji na kushindwa kukidhi ubora.

"Asilimia 80 ya wafugaji wa kuku wa nyama ni wanawake, nawataka kushikilia tasnia hiyo ili kuondoa umasikini kuanzia ngazi ya familia hadi taifa," alisema Sichwale.

# Ataka kuku Dar, Pwani kuuzwa kwa kilo

Na Mwandishi Wetu

**W**AZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameagiza wafanyabiashara wa kuku Dar es Salaam na Pwani wauze mifugo hiyo kwa kilo na wawe na umoja kwenye hilo.

Ameagiza wafakaokiuwa agizo hilo washughulikiwe na akatoa pia msimamo kuwa serikali haiwezi kuweka bei elekezi ya nyama.

Aliyasema hayo wakati wa mktano wa wazalishaji na wafugaji wa kuku katika mkoa wa Dar es Salaam juzi. Ndaki alisema kwa kipindi kirefu sekta ya ufugaji wa kuku imekuwa ikichezewa na hivyo kuwaathiri wafugaji.

"Anzeni kuuza kuku kwa kilo kuanzia sasa, wekeni utaratibu mkubaliane katika vyama vyenu na mkubaliane kuuza kuku kwa kilo... atakayekwenda kinyume hapo mnawenza kumshughulikia kwa utaratibu wenu," alisema.

Ndaki alisema haileti maana kuona nyama ya ng'ombe, mbuzi, samaki na zinginezo zikiuzwa kwa kilo halafu kuku ambaye ni kitoweo muhimu auzwe kwa kukadiria hivyo kutokuwa na tija kwa mfugaji.

Alisema serikali imeanza utaratibu wa kuweka mizani katika maeneo yote ya uuzaji wa mifugo ikiwemo minadani ili kuwapima wanyama kabla ya kuwauza.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, alisema wilaya hiyo imetenga Sh bilioni nné kukopesha vikundi vya wajasiriamali wa sekta ya nyama na kuwataka wajitokeze ili waweze kuinua mitaji yao.